# Lyandiko lya mwaluko lya Wandewa

## Chilongole

Vitabu vya 1 Wandewa na 2 Wandewa aho hamwande navyali chitabu chimwe chikulu. Nachigawanulwa kuli vitabu vili kuli Seputuajenti, navilavigwa katali ng'hatu na ndo Ilagano lya Katali kuli ndonga ya Chigilichi cha katali. Hailinguzeleka whaani yandiche vitabu avi vya 1 Wandewa na 2 Wandewa ama kuviwika kuli koneka aku. Munhu yandiche vitabu vya Wandewa nakatumiya kalatasi zimwenga za katali kuli kuvyandika (ulole 1 Wandewa 11:41, 14:19 na 14:29). Hailinguzeleka kahi kota nili vitabu avi navyandichigwa na kuwichigwa goya. Ndo kukomya kota nawasinda kwandika na kuviwika goya kulawa loyalechelwe mndewa Yekoniya kulawa kuli isi ya chijenzi ako Babuloni, kuli mwaka wa 561 Yesu yang'hali kupondigwa, kwa vila mbuli ayi naisimilwa kuli 2 Wandewa 25:27. Wasomile wenji wa mbuli zilinguwala Bibiliya wangijesa kota honhu hakulu ha vitabu avi nahandichigwa miyaka minji loung'hali mhela awo.

Vitabu vya 1 Wandewa na 2 Wandewa vyangusimila mbuli za chila mndewa wa Isilaeli na Yuda kulawa kuli mhela wa ulongozi wa Solomoni, mhela wanhu wa isi azi mbili vyowawele wang'hali welumbile. Vitabu vya 1 Wandewa na 2 Wandewa vyangusimila ndaze undewa

wa Isilaeli ilumbile vyougawanuche na kuwa kuli banzi mbili, ziwele nazali ziwinza mbuli zilivinji, mbaka hala banzi azi mbili vyozilemwele na wanhu wake kuhilikwa kuli isi za chijenzi. Yalingwandika kangumpugajiza chila mndewa leka yavizele kota nayali yomuwinza Nguluwi kwa kukomya ama hebu. Wandewa wamwe “nawadita ganojile hali Mkulu Nguluwi” (2 Wandewa 18:3). Wanji “nawadita gehile hali Mkulu Nguluwi” (2 Wandewa 21:2). Yalingwandika kangusimila ng'hatu mbuli za ulongozi wa wandewa waditile ganojile hali Mkulu Nguluwi na kulajila kota mbuli zilingulutilila goya kuli chila wanhu wa isi zangulawa kuli kukundigwa kwa mndewa hali Nguluwi. Kuli 2 Wandewa 17:7, twangusoma kota Waisilaeli nawaholigwa na kuhilikwa kuli isi ya chijenzi kwa vila “Waisilaeli nawadita gehile hali Mkulu Nguluwi” na kwa vila “nawajifugamila milungu.”

**Gali mgati ga kuli 1 Wandewa**

1. Sula ya 1-11 zangusimila ndaze Solomoni, mwana wa Daudi vyoyawele mndewa na mbuli za ulongozi wa heye wa Isilaeli ilumbile.
2. Kuli sula ya 12-16 twangusoma kuwala kugawanuka kwa undewa wa Isilaeli na Yuda na wandewa wamwenga wa wanhu wa isi azi mbili.
3. Sula ya 17-19 zangusimila mbuli za mijito ja mloli Eliya na kuwala nhing'hano ziwele hali heye Eliya na mndewa Ahabu wa Isilaeli.
4. Sula ya 20-22 zangusimila kuwala kuduma kwa ulongozi wa mndewa Ahabu kuli Isi-

laeli na mbuli za wandewa wanji wawele nawalongoza vyoudumile ulongozi wa heye, hamwe na mbuli za wandewa wa Yuda.

### *Mazuwa ga kuduma ga mndewa Daudi*

1 Mhela mndewa loyawele sekulu ng'hatu, vitu-
magwa wa heye nawamgubika kwa migolole, ila
hawezile kupata ivuche.
2 Ahyo nawamlonjela, “Mkulu wa hetwe mn-
dewa, fola tukupalile mhinza yakukolele mijito
na kukulolela na kuwasa hamwe na hegwe leka
yakupe ivuche.”
3 Hamba nawapala mhinza yalingoneka
yanojile kuli isi yeng'ha ya Isilaeli, nawampata
mdala yumwe yanojile yalinguchemigwa
Abishagi, Mshunami, nawamigala kwa mndewa.
4 Mdala ayo nayali yokoneka yanojile lukami.
Lelo nakaluka kumkolela mijito na kumlolela mn-
dewa. Mndewa nakawasa na yula mhinza, ila
kwa chiwalo cha ivuche hela.

### *Adoniya kangipalila undewa*

5 Mhela awo, Adoniya, yawele mayake ndo Hag-
iti, nakaluka kidaya na kulonga, “Ndowa mn-
dewa.” Lelo nakalajiza yawichilwe goya mituka ja
kubulunwa na falasi na wakwina falasi na wamizi
makumi gahano walingulongola kuno wobilima.
6 Ila kulawa Adoniya loyapondigwe, mhaza
wa heye Daudi, hamng'hanuchile mwanage ne
zuwa limwe ne kumuuza, “Lekachoni kwangu-
dita ahyo?” Adoniya nayali yokoneka yano-
jile ng'hatu, nakapondigwa Abusalomu, hamba
nakapondigwa heye.

7 Adoniya nakalongasa na Yoabu, mwana wa
Seluiya na mtambika Abiatali, nawo nawakunda
kumuwinza na kumtanza heye.
8 Ila mtambika Sadoki na Benaya, mwana wa
Yehoyada na mloli Natani na Shimeyi na Leyi,
hamwe na wamizi wa chiuyeng'ha wa Daudi,
hawakundile kumuwinza Adoniya.
9 Zuwa limwe, Adoniya nakalavya nhambiko ya
ing'holo na isenga na milogota jinonile kuli honhu
halinguchemigwa Iganga lya Izoka, habehi na
nzasa ilinguchemigwa Eni-logeli. Nakawalalika
wakalumbu wa heye kuli mnvina ya nhambiko
ayo wawele ndo wana wanji wa mndewa na vilon-
gozi weng'ha wa nhanzi ya Yuda,
10 ila hawalaliche mloli Natani na Benaya na
wamizi wa chiuyeng'ha wa mndewa Daudi na
Solomoni mng'holoze.

### *Solomoni kanguwichigwa yawe mndewa*

11 Aho ndo Natani nakaluta kwa Batisheba,
mayake Solomoni, nakamuuza, “Ndaze,
hauhuliche kota Adoniya, mwana wa Hagiti
nakeholela ludali lwa mndewa na mkulu wa
hetwe Daudi ne heye kuvizela?
12 Lelo, ubeteze ndikulonjele ndaze vyouweza
kuulohola ukomu wa hegwe na wa mwanago
Solomoni.
13 Ulute kwa mndewa Daudi na umuuze,
‘Mkulu wa heni mndewa, ndaze hundahile
heni chitumagwa wa hegwe ulonga, “Ndikomya,
mwanago Solomoni kolongoza honhu ha heni na
kochikalisa kuli chigoda cha heni cha undewa?”
Naiwa ndaze lelo Adoniya nakawa mndewa?’

14 Louwa ulutilila kulongasa na mndewa, heni
ndokwinjila na kutawiza ulonzi wa hegwe.”

15 Lelo, Batisheba nakaluta kumlola mndewa
kuli chihengo cha heye, honhu hawele Abishagi,
Mshunami nayali yomkolela mijito. Mhela awo
mndewa nayali sekulu lukami.
16 Batisheba nakamfugamila mndewa
kwa kumhulichiza, mndewa nakamuuza,
“Kwangugana choni?”
17 Batisheba nakedichila, “Mkulu wa heni, naw-
ilaha hali heni, chitumagwa wa hegwe na hali
Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa hegwe, ulonga,
‘Mwanago Solomoni kolongoza honhu ha heni na
kochikalisa kuli chigoda cha hegwe cha undewa.’
18 Ila lehano, Adoniya nakawa mndewa, nagwe
huvizelele.
19 Nakalavya nhambiko ya misenga na milo-
gota jinonile na ming'holo na kuwachema wana
weng'ha wa mndewa na mtambika Abiatali na
Yoabu, chilongozi wa wamizi, ila chitumagwa wa
hegwe Solomoni hamchemile.
20 Lelo, mkulu wa heni mndewa, Waisilaeli
weng'ha wangukubeteza leka uwalonjele munhu
yawele kochikalisa kuli chigoda cha hegwe cha
undewa, honhu ha hegwe.
21 Wone haiwa ahyo, mhela hegwe mndewa wa
heni houbagama, heni hamwe na mwana wa heni
Solomoni toditilwa vibi kota wabelenhuche.”
22 Mhela Batisheba loyawele yolutilila kulon-
gasa na mndewa, mloli Natani nakenjila kuli
ng'handa ya mndewa.
23 Wanhu nawamlonjela mndewa, “Mloli
Natani ka hano.” Naye loyamfichile mndewa

nakamfugamila mndewa mbaka kumeho kwa heye nakudoliza hasi.

24 Aho ndo Natani nakalonga, “Mkulu wa heni, ndaze, nakulonga, ‘Adoniya kolongoza honhu ha heni na kochikalisa kuli chigoda cha heni cha undewa?’

25 Kwa vila lehano nakaluta kulavya nhambiko ya misenga na milogota jinonile na ming'holo na kuwalalika wana wa mndewa na Yoabu, mkulu wa wamizi na mtambika Abiatali. Ulole, wangulya na kunwa hali heye na kulonga, ‘Wikale mhela winji mndewa Adoniya.’

26 Ila hanyhemile heni, chitumagwa wa hegwe ne mtambika Sadoki ne Benaya, mwana wa Yehoyada ne chitumagwa wa hegwe Solomoni.

27 Ndaze, aga geng'ha nakugakola gwegwe mndewa wa heni ne kutulonjela vitumagwa wa hegwe, munhu yawele kochikalisa kuli chigoda cha hegwe cha undewa honhu ha hegwe?”

28 Mndewa Daudi nakamlonjela “Nyhemele Batisheba.” Batisheba nakaluta kwa mndewa na kwima hali heye.

29 Hamba mndewa nakelaha, yolonga, “Kota Mkulu Nguluwi vyoyalingikala, yawele nakangombola kulawa kuli magazo menji,

30 kota vyondikulahile hali Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa Isilaeli, kuno ndilonga, ‘Mwanago Solomoni kolongoza honhu ha heni na kochikalisa kuli chigoda cha heni cha undewa honhu ha heni,’ ndo vyondidita lehano.”

31 Batisheba nakamfugamila mndewa kwa kumhulichiza na kulonga, “Mkulu wa heni, mndewa Daudi, wikale mhela winji!”

32 Hamba mndewa Daudi nakalonga,
“Nyhemele mtambika Sadoki na mloli Natani na
Benaya, mwana wa Yehoyada.” Nawo nawaluta
kwa mndewa.
33 Mndewa nakawalonjela, “Mlute na
vitumagwa wa heni, mumuwiche mwana wa
heni Solomoni mchanya mwa igongolo lya heni,
mumhiliche Gihoni.
34 Lomuwa ako, mtambika Sadoki na mloli
Natani wambakalize mafuta leka yawe mndewa
wa Isilaeli, hamba mpembe mhalamhanda na ku-
longa, ‘Mndewa Solomoni yekale mhela winji!’
35 Namwe moluta hamwe na heye, naye
kochikalisa kuli chigoda cha heni cha undewa
honhu ha heni. Nandimuwika yawe chilongozi
kuli Isilaeli na kuli Yuda.”

36 Aho ndo Benaya, mwana wa Yehoyada
nakamwidichila mndewa, “Ena! Mkulu Nguluwi,
Nguluwi wa mndewa wa heni, yalonje hihyo du.
37 Kota vila vyoyawele Mkulu Nguluwi na mn-
dewa wa heni, Solomoni kahi yawe hihyo. Mkulu
Nguluwi yachidite chigoda cha heye cha undewa
chiwe chikulu kusinda chila cha mndewa wa heni
Daudi.”

38 Ahyo, mtambika Sadoki na mloli Natani na
Benaya, mwana wa Yehoyada na Wakeleti na
Wapeleti, nawamkwiniza Solomoni kuli igongolo
lya mndewa Daudi, liwele kota idogowi likulu,
nawamhilika mbaka Gihoni.
39 Hamba mtambika Sadoki nakahola mbalati
ziwele na mafuta kulawa kuli honhu ha kulavila
nhambiko na kumbakaliza Solomoni leka yawe
mndewa. Hamba nawapemba mhalamhanda na

wanhu weng'ha nawalonga, “Mndewa Solomoni
yekale mhela winji!”
40 Hamba wanhu weng'ha nawamuwinza
wopemba mhalamhanda, nawasangalala kwa
mnvina ng'hulu na isi naitigasika kwa chiwalo
cha lizi lya hewo.
41 Lelo, Adoniya hamwe na weng'ha wawele
hamwe na heye nawahulika lizi alyo lowawele
wosinda mnvina ya hewo. Lowahuliche lizi lya
mhalamhanda, Yoabu nakauza, “Iyowe alyo ako
mujini ndo lya choni?”
42 Loyawele yolonga, Yonatani mwana wa
mtambika Abiatali nakenjila, hamba Adoniya
nakalonga, “Winjile, kwa vila hegwe ndo munhu
yanojile, kwangigala mbuli inojile.”
43 Yonatani nakamwidichila Adoniya, “Hebu!
Mndewa Daudi nakamdita Solomoni yawe mn-
dewa.
44 Mndewa nakamlajiza mtambika Sadoki na
mloli Natani na Benaya, mwana wa Yehoyada
na Wakeleti na Wapeleti, nawo nawamkwiniza
mchanya mwa igongolo lya mndewa,
45 hamba mtambika Sadoki na mloli Natani
nawambakaliza mafuta leka yawe mndewa kula
Gihoni. Kwaluchila aho nawalutilila kusangalala
na lizi nalyenela kuli muji weng'ha. Alyo ndo lizi
lyoulingulihulika.
46 Sambi Solomoni nakekalisa kuli chigoda cha
heye cha undewa.
47 Mzidi ya ago, vitumagwa wa mndewa
nawoya kumtogola mkulu wa hetwe, mndewa
Daudi kuno wolonga, ‘Nguluwi wa hegwe yalidite
itagwa lya Solomoni lizeleche kusinda lya

hegwe na chigoda cha heye cha undewa chiwe
chikulu kusinda cha hegwe.’ Hamba mndewa
nakafugama mchinhanda mwa heye,
48 nakalanda yolonga, ‘Yatogoligwe Mkulu Ngu-
luwi, Nguluwi wa Isilaeli, yawele nakakunda
meho ga heni kumona yalinguhalila chigoda cha
heni cha undewa lehano.’ ”
49 Lelo, wanhu weng'ha wawele hamwe na
Adoniya nawadumba ng'hatu na kusambaluka.
50 Kwa vila Adoniya nakamdumba Solomoni,
nakaluta kibata mbalati za kuli honhu ha kulavila
nhambiko leka yelohole.
51 Hamba mndewa Solomoni nakahulika kota
Adoniya nayali yabilimile kuli ihema na kibata
mbalati za kuli honhu ha kulavila nhambiko yo-
longa, “Sikuka hano mbaka mndewa Solomoni
yandonjele kota sikopoligwa.”
52 Mndewa Solomoni nakalonga, “Wone kochi-
lajila kota ka yalingukundigwa, hoditigwa chinhu
choneche. Ila wone ndimone kota ndo mwihe,
yomlapa yabagame.”
53 Lelo mndewa Solomoni nakawalajiza wanhu
wamigale Adoniya kulawa kuli honhu ha kulavila
nhambiko. Adoniya nakoya na kinamiza hali mn-
dewa Solomoni. Mndewa nakamlonjela, “Ulute
haluga ha hegwe.”

# 2

*Daudi kangumlajiza Solomoni*

1 Daudi loyawele habehi kubagama, nakam-
chema Solomoni mwanage na kumlonjela,

2 “Mwanangu, kota vyoilinguzeleka,
vilumbigwe vyeng'ha vyobagama, mazuwa ga
heni nagamala. Wime nzinzili na uwe uzidahe.
3 Weneze malajizo ga Mkulu Nguluwi, Nguluwi
wa hegwe, uwinze nzila za heye na kibatilila
mizilo ja heye na malajizo ga heye na nhaguso
za heye na ulolezi wa heye, kota vyoyandichigwe
kuli malajizo ga Musa, leka mbuli za hegwe zilu-
tilile goya koneche kouluta,
4 leka Mkulu Nguluwi yeneze kulagana kwa
heye, loyandonjele, ‘Wone walelwa wa hegwe
wobatilila mizilo ja heni na kung'holela mijito
kwa kukundigwa na kwa nhumbula yeng'ha,
kowa na munhu hali hemwe yawele kochikalisa
kuli chigoda cha undewa cha Isilaeli.’
5 “Mzidi wa ago, kwangugazela gala goyandi-
tile Yoabu, mwana wa Seluiya, vila vyoyawadi-
tile wakulu wa wamizi weli wa Isilaeli, wawele
ndo Abuneli, mwana wa Neli na Amasa, mwana
wa Yeteli. Nakawakopola, nakabohola danda ya
hewo mhela wa kikala goya kota vila kuli ngondo,
kahi nayali na nongwa kwa vila nakaibakaliza
danda yila kuli isali liwele kuli chuno cha heye na
makwamba gawele goyavalile.
6 Umditile vyoulinguweza kwa luhala lwa
hegwe, ila uleche kumleka yabagame kwa kikala
goya.
7 “Ila uwalajile igano lya kwimilila wana wa
Balisilayi, Mgileadi na uwakundize wawe hali
wala walingulya kuli chisaga cha hegwe, kwa vila
nawanditila igano lya kwimilila mhela lombele
ndibilima kwa chiwalo cha mng'holozo Abusa-
lomu.

8 Kabaho kahi Shimeyi, mwana wa Gela,
Mbenjamini wa Bahulimu, yawele nakamhanjila
lukami londutile Mahanaimu. Vyoyoyile
kunhing'haniza kuli lwanda lwa Yolodani
nandimlahila kwa itagwa lya Mkulu Nguluwi
ndimlonjela, ‘Sikukopola kwa ipanga.’
9 Ila lelo, uleche kijesa kota kahela nongwa.
Hegwe kuna luhala kovizela choumditila, uleche
kumleka yabagame kwa kikala goya.”

### *Kubagama kwa Daudi*

10 Hamba Daudi nakabagama, nakatiligwa
Yelusalemu, kuli muji wa heye.
11 Mhela Daudi woyalongoze Isilaeli nawali
miyaka makumi gane. Ako Hebuloni nakalon-
goza kwa miyaka saba na Yelusalemu nakalon-
goza kwa miyaka makumi gadatu na jidatu.
12 Lelo Solomoni nakekalisa kuli chigoda cha
undewa honhu ha Daudi, mhaza wa heye na un-
dewa wa heye nawima nzinzili.

### *Kubagama kwa Adoniya*

13 Hamba Adoniya, mwana wa Hagiti, nakaluta
kwa Batisheba, mayake Solomoni. Batisheba
nakamuuza, “Ndaze, kwanguya kwa kikala
goya?” Adoniya nakamwidichila, “Ena, ndanguya
kwa kikala goya.”
14 Hamba nakalonga, “Ndina mbuli imwe
hela ya kukulonjela.” Batisheba nakamlonjela,
“Ulonje.”
15 Adoniya nakamlonjela, “Kota vyoulingu-
vizela, undewa nawali wa heni. Waisilaeli
weng'ha nawali wondola kota ndo mndewa wa
hewo. Ila mbuli nazigaluka, undewa nauluta kwa

mng'holozangu, Mkulu Nguluwi nakagana mbuli ayi iwe kota vyoilawile.
16 Lelo ndangukulanda chinhu chimwe, ndangukudedeza uleche kundemela." Batisheba nakamlonjela, "Longa."
17 Nakalonga, "Dedede ndangukulanda umlande mndewa Solomoni, yamhe heni Abishagi, Mshunami, yawe mche wangu, howeza kulema."
18 Batisheba nakamlonjela, "Goya, ndolongasa na mndewa honhu ha hegwe."
19 Lelo Batisheba nakaluta kulongasa na mndewa Solomoni kwa chiwalo cha Adoniya. Mndewa nakenuka nakaluta kumbochela mayake, nakafugama, hamba nakekalisa kuli chigoda cha heye cha undewa. Nakalajiza chigoda cha undewa chigaligwe kwa heye kwa chiwalo cha mayake, naye mayake nakekalisa kuli moko wa kudilo wa mndewa.
20 Batisheba nakamlonjela mndewa, "Ndina mbuli nyindo ndangukulanda, dedede uleche kundemela." Mndewa nakamlonjela, "Longa mayangu, sikulemela."
21 Mayake nakalonga, "Mkundize mng'holozo Adoniya yamhole Abishagi, Mshunami leka yawe mche wake."
22 Mndewa Solomoni nakamuuza mayake, "Lekachoni kwangumlanda Abishagi, Mshunami, kwa chiwalo cha Adoniya? Mbuli ayi naiwhana ng'hatu na kumganila undewa wa heni, kwa vila heye ndo mkulu kwa heni na kwa vila Yoabu, mwana wa Seluiya na mtambika Abiatali wa hamwe na heye."
23 Aho mndewa Solomoni nakelaha kwa

itagwa lya Mkulu Nguluwi yolonga, “Nguluwi
yang'hopole ne kumbonela isungu, wone Adoniya
hobagama kwa chiwalo cha kulanda aku!
24 Lelo, ndangilaha kwa itagwa lya Mkulu Ngu-
luwi yawele mkomu, yawele nakambika na kun-
yimiza nzinzili kuli undewa wa mhaza wa heni
Daudi na yawele nakeneza kulagana kwa heye
kwa kumha undewa heni na lulelo lwa heni,
ndikomya, Adoniya kobagama!”
25 Aho ndo mndewa Solomoni nakamlajiza Be-
naya, mwana wa Yehoyada, naye Benaya naka-
luta kwa Adoniya na kumkopola.

### *Abiatali kanguwinjigwa na Yoabu kangukopoligwa*

26 Mndewa Solomoni nakamlonjela mtambika
Abiatali, “Ulute ako Anatoti kuli migunda
ja hegwe. Kwangulapigwa kubagama, ila
sikukopola sambi kwa vila nakulihola isanduku
lya ilagano lya Mkulu Nguluwi hali mhaza wa
heni Daudi na kugazigwa hamwe na heye.”
27 Ahyo mndewa Solomoni nakamuwinga Abi-
atali kuli utambika wa Mkulu Nguluwi, yok-
weneza ulonzi wa Mkulu Nguluwi woyalonjile
ako Shilo, galingumuwala Eli na lukolo lwa heye.
28 Yoabu loyahuliche mbuli azo, nakabilim-
ila kuli ihema lya Mkulu Nguluwi na kibatilila
mbalati za honhu ha kulavila nhambiko, kwa
chiwalo cha kikala goya. Nakadita ahyo kwa
vila nayali yelumbile na Adoniya, ila hawele na
Abusalomu.
29 Mndewa Solomoni loyahuliche kota Yoabu ka
kuli ihema lya Mkulu Nguluwi na nayali yemile

habehi na honhu ha kulavila nhambiko, nakamla-
jiza Benaya, mwana wa Yehoyada, yolonga, “Ulute
ukamtowe.”
30 Benaya nakaluta kuli ihema lya Mkulu Ngu-
luwi, nakamlonjela Yoabu, “Mndewa kanguku-
lonjela, ‘Ulawe amo.’ ” Yoabu nakedichila, “Hebu,
ndobagama bahano.” Benaya nakahiluka kwa
mndewa na kumlonjela vyoyalonjile Yoabu.
31 Mndewa Solomoni nakamlonjela Benaya,
“Udite kota vyoyalonjile. Umtowe na kumtila,
leka kusa gehile kulawa kwa heni na ivyazi lya
mhaza wa heni, gehile ga danda ilihela nongwa
iwele naiboholigwa na Yoabu.
32 Mkulu Nguluwi komgaza Yoabu kwa
kukopola ako koyaditile ne mhaza wa heni Daudi
kuvizela. Nakawakopola kwa ipanga wanhu weli
wawele watanganiche kusinda heye na nawali
wanojile kusinda heye. Nakawakopola Abuneli,
mwana wa Neli, mkulu wa wamizi wa Isilaeli na
Amasa, mwana wa Yeteli, yawele nayali mkulu
wa wamizi wa Yuda.
33 Nongwa ya kubohola danda iwe kwa Yoabu
na walelwa wa heye mazuwa gose. Ila kwa Daudi
na walelwa wa heye na ivyazi lya heye na chigoda
cha heye cha undewa, wawe na kikala goya kwa
Mkulu Nguluwi mazuwa gose.”

34 Lelo Benaya, mwana wa Yehoyada, naka-
luta kuli ihema nakamtowa Yoabu na kumkopola,
nakatiligwa kuli mgunda wa heye kuchiwala.
35 Mndewa nakamuwika Benaya, mwana wa
Yehoyada, yawe mkulu wa wamizi honhu ha
Yoabu na Sadoki yawe mtambika honhu ha Abi-
atali.

## *Kubagama kwa Shimeyi*

36 Hamba mndewa nakalajiza usenga kwa
Shimeyi na kumlonjela, “Wizenjele ng'handa
amu Yelusalemu, wikale aha ila uleche kuluta
honhu hanji.
37 Zuwa loukuka na kuloka ibindi lya Kidiloni,
ndangukulonjela ndikomya kota kobagama kwa
kiyambuza gwegwe baho.”
38 Shimeyi nakamwidichila mndewa, “Goya
mndewa. Ndodita kota mkulu wa heni, mn-
dewa vyoulonjile.” Lelo nakekala Yelusalemu
kwa mhela winji.

39 Ila kuli kuduma kwa mwaka wa kadatu, wa-
pogozi weli wa Shimeyi nawasulupuka na kuluta
kwa Akishi, mwana wa Maaka, mndewa wa Gati.
Shimeyi loyahuliche kota wapogozi wa ako Gati,
40 nakakwina idogowi lya heye nakaluta
kuwapala ako Gati kwa mndewa Akishi. Lelo,
nakawafika ako na nakawahilula kaye.
41 Mndewa Solomoni loyahuliche kota Shimeyi
nayali yochile Yelusalemu, nakaluta Gati na
kuhiluka,
42 mndewa nakamchema Shimeyi na kumuuza,
“Ndaze, hundahile kwa itagwa lya Mkulu Ngu-
luwi kota hulawa Yelusalemu, nani sikukany-
ile kota kobagama wone kojeza kuluta kunze?
Nagwe nakukunda na kundonjela, ‘Goya, ndo-
hulichiza.’
43 Lekachoni lelo nakubena chilaho chowilahile
kwa Mkulu Nguluwi na kubena mzilo wondiku-
pele?”
44 Mndewa nakalutilila kumlonjela Shimeyi,
“Kwangugazela gehile goumditile mhaza wa heni

Daudi, lelo kwa chiwalo cha ago, Mkulu Nguluwi kokugaza.
45 Ila heni Solomoni ndotambichizwa na chigoda cha undewa cha Daudi chokwimizwa nzinzili hali Mkulu Nguluwi mazuwa gose."
46 Hamba, mndewa nakamlajiza Benaya, mwana wa Yehoyada, naye nakalawa na kumtowa Shimeyi na kumkopola. Lelo, undewa wa Solomoni nawali wimile nzinzili.

# 3

*Solomoni kangulanda luhala*

1 Solomoni nakelumba na Falao, mndewa wa Misili na kumhesa mhinza wa heye. Nakamhilika mhinza wa Falao na kumuwika kuli Yelusalemu, muji wa Daudi, mbaka loyasindile kuzenga ng'handa ya heye ya chiundewa na ng'handa ya Mkulu Nguluwi, hamwe na lukanzi lulinguzunguluta muji wa Yelusalemu.
2 Wanhu nawali wolutilila kulavya nhambiko kuli honhu halivinji ha kufugamila, kwa vila ng'handa ya Mkulu Nguluwi nayali ing'hali kuzenjigwa.
3 Solomoni nakamgana Mkulu Nguluwi, nayali yowinza mizilo ja Daudi, mhaza wa heye, ila heye nakalavya nhambiko na kufunyiza ubani ako hali honhu ha kufugamila.
4 Mhela umwenga, mndewa Solomoni nakaluta kulavya nhambiko ako Gibeoni, honhu aho nahali honhu ha kufugamila halinguzeleka lukami, naye Solomoni nakalavya nhambiko za kulakazwa elufu imwe mchanya mwa honhu aho ha kulavila nhambiko.

5 Mkulu Nguluwi nakamlawila Solomoni ako
Gibeoni, kuli kulota mhela wa nechilo, Ngu-
luwi nakamlonjela, “Undande choneche nani
ndokupa.”
6 Solomoni nakalonga, “Nakumlajila igano lya
kwimilila chitumagwa wa hegwe Daudi, mhaza
wa heni, kwa vila nakakukolela mijito kwa
kukundigwa na kwa hachi na kwa nhumbula
igoloche. Nakulutilila kumlajila igano lya
kwimilila kwa kumha mwana wa kikalisa kuli
chigoda cha heye cha undewa.
7 Lelo, gwa Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa
heni, nakumbika heni chitumagwa wa hegwe
ndiwe mndewa honhu ha mhaza wa heni Daudi.
Ila nding'hali mwana mdodo sivizelele ndaze
vyondilinguganigwa kulongoza.
8 Nakumbika aha hali wanhu wa hegwe
wawele nakuwahagula, wanhu wenji wohambe
wawazigwe ne kuizela hisabu ya hewo.
9 Ahyo, ndangukulanda umhe heni chitumagwa
wa hegwe uwanzi leka ndiwalongoze wanhu wa
hegwe na kuvizela ganojile na gehile. Whaani
yoweza kuwalongoza awa wanhu wa hegwe
wawele wenji ahi?”
10 Kulanda aku kwa Solomoni nakumnojeza
Mkulu Nguluwi.
11 Nguluwi nakamlonjela, “Kwa vila nakulanda
mbuli ayi, hulandile kwa chiwalo cha kikala
mazuwa menji ama lufufu ne kulanda kwa chi-
walo cha kubagama kwa wang'honyo wa hegwe,
ila nakulanda kuvizela kwa chiwalo cha hegwe
kutagusa kwa hachi,
12 lelo ndodita kota vyoulandile. Ndokupa

uwanzi na luhala, chasi chiwele hanalawila munhu yunji kota hegwe na howeza kulawila hamba.
13 Mzidi wa ago, ndokupa gala gawele hun-
dandile, gawele ndo lufufu na lutogo, leka kuli kikala kwa hegwe kweng'ha hakuweza kulawila munhu kota hegwe hali wandewa.
14 Wone kowinza nzila za heni na kibatilila
mizilo ja heni kota vyoyaditile mhaza wa hegwe Daudi, ndokutambichiza leka wikale mazuwa menji."
15 Solomoni loyenuche nakavizela kota nay-
ali yolota. Nakahiluka Yelusalemu, nakema kumwando mwa isanduku lya ilagano lya Mkulu Nguluwi na kulavya nhambiko za kulakazwa na za kikala goya. Hamba nakawaditila mnvina vitumagwa wa heye weng'ha.

### *Luhala lwa Solomoni lwangoneka kuli nhaguso*

16 Zuwa limwe wadala weli wang'hondwa
nawaluta kwa mndewa Solomoni na kwima hali heye.
17 Yumwe wa hewo nakalonga, "Gwa mkulu wa
heni, heni na ayu myangu twangikala ng'handa imwe. Heni namhonda mwana, mhela ayu loyawele hamwe na heni.
18 Mazuwa meli hamba kulawa loyapondigwe
ayu mwana wa heni, ayu naye nakaponda mwana. Natwali twetwe yeka, hakuwele na yoneche kuli ng'handa ayo, ila hetwe weli hela.
19 Zuwa limwe nechilo mwanage nakabagama,
kwa vila nayali yamuwasile.
20 Loyenuche nechilo ayo, nakamhola mwana
wa heni mhela heni lombasile. Nakamuwasiliza

hali mhambaga ya heye na kumuwika mwanage
yabagame kuli mhambaga ya heni.
21 Lonyinuche hamitondo kumonyeza mwana
wa heni, nandimona yawele yabagame. Ila londo-
lile ng'hatu nandivizela kota hawele yula mwana
wa heni yondimpondile."
22 Ila yula mdala yunji nakalonga, "Hebu.
Mwana yawele mkomu ndo wa heni na yabagame
ndo wa hegwe." Naye mdala wa mwaluko naka-
longa, "Hebu. Mwana yawele mkomu ndo wa
heni na yabagame ndo wa hegwe." Ahi ndo vy-
owawele wochitwanza hali mndewa.
23 Mndewa Solomoni nakalonga, "Chila yumwe
wa hemwe kangulonga kota mwanage ndo
yawele mkomu, yabagame hawele wa heye."
24 Lelo mndewa nakalajiza, "Mngalile ipanga."
Nawamigalila mndewa ipanga.
25 Mndewa nakalonga, "Mdumule ayo mwana
yawele mkomu kuli vihande vili, umhe mdala ayu
nusu na mdala yunji kahi nusu iyage."
26 Yula mdala yawele mwanage ndo yawele
mkomu, nayali yamemile isungu kwa chiwalo
cha mwanage na kumlonjela mndewa, "Dedede
mkulu wa heni, uleche kumkopola mwana. Umhe
heye mwana ayu yawele mkomu." Ila yula mdala
yunji nakalonga, "Yadumuligwe kuli vihande vili,
leka yaleche kuwa wa heni ne wa hegwe!"
27 Hamba, mndewa Solomoni nakalonga,
"Mumhe mdala wa mwaluko mwana yawele
mkomu. Mleche kumkopola, ayo ndo mayake."
28 Wanhu weng'ha wa Isilaeli lowahuliche uta-
guso woyaulavile mndewa, nawamdumba mn-
dewa, kwa vila nawona kota nayali na luhala

kulawa kwa Nguluwi kwa kulavya hachi.

# 4

### *Vilongozi wa Solomoni*

1 Solomoni nayali mndewa wa isi yeng'ha ya
Isilaeli.
2 Wano nawali wamwe wa vilongozi wa heye
wakulu. Asaliya, mwana wa Sadoki, nayali mtam-
bika.
3 Eliholefu na Ahiya wana wa Shausha, nawali
walingwandika. Yehoshafati, mwana wa Ahiludi,
nayali yalingwandika kukumbuchila.
4 Benaya, mwana wa Yehoyada, nayali chilon-
gozi wa wamizi na Sadoki na Abiatali, nawali
watambika.
5 Asaliya, mwana wa Natani, nayali chilongozi
wa wakulu wa mikowa na mtambika Sabudi,
mwana wa Natani, nayali goloko wa mndewa.
6 Ahishali, nayali mkulu wa ng'handa ya mn-
dewa na Adonilamu, mwana wa Abuda, nayali
yalingulolela mijito ja kukola lupichi.
7 Solomoni nayali kahi na vilongozi kumi na
weli kuli isi yeng'ha ya Isilaeli. Awo nawapegwa
mijito ja kuwinza chilyo kwa chiwalo cha mn-
dewa na kwa chiwalo cha wanhu wa ng'handa ya
heye mndewa. Chila yumwe wa hewo nakegala
chilyo kwa mwezi umwe kuli chila mwaka.
8 Aga ndo matagwa ga vilongozi, Beni-huli,
nakalongoza isi ya vidunda vya Efulaimu
9 na Beni-dekeli, nakalongoza miji ja Makasi
na Shaalibimu na Beti-shemeshi na Eloni-beti-
hanani.

10 Beni-hesedi nayali chilongozi wa muji wa
Aluboti na Soko na isi yeng'ha ya Hefeli.
11 Beni-abinadabu, mlume wa Tafati, mhinza
wa Solomoni, nakalongoza isi yeng'ha ya Nafoti-
doli.
12 Baana, mwana wa Ahiludi, nakalongoza miji
ja Taanaki na Megido na honhu heng'ha ha Beti-
sheani iwele habehi na muji wa Saletani, kusini
mwa muji wa Yesileeli na kulawa Beti-sheani
mbaka muji wa Abeli-mehola mbaka kupuluta
muji wa Yokimeamu.
13 Beni-gebeli nakalongoza muji wa Lamoti-
gileadi hamwe na vijiji vya Gileadi viwele kuli isi
ya Yaili, mlelwa wa Manase. Nakalongoza kahi
mkowa wa Aligobu, uwele Bashani, najali miji
mikulu makumi sita jizungulusilwe lukanzi na
kuwichilwa fito za shaba kuli lwizi.
14 Ahinadabu, mwana wa Ido, nakalongoza
muji wa Mahanaimu.
15 Ahimaasi, mlume wa Basemati, mhinza wa
Solomoni, nakalongoza isi ya Nafutali.
16 Baana, mwana wa Hushayi, nakalongoza isi
ya Asheli na Bealoti.
17 Yehoshafati, mwana wa Palua, nakalongoza
isi ya Isakali.
18 Shimeyi, mwana wa Ela, nakalongoza isi ya
Benjamini.
19 Gebeli, mwana wa Uli, nakalongoza isi ya
Gileadi, ndo yila iwele naiholigwa na Sihoni, mn-
dewa wa Waamoli na Ogu mndewa wa Bashani.
Mzidi wa awa kumi na weli, nakwali na mkulu
yumwe yawele nayali yolongoza isi yeng'ha.

### *Ulongozi wa Solomoni wangulutilila goya*

20 Wanhu wa Yuda na wa Isilaeli nawali wenji
kota sangalaza za mhwani, nawalya na kunwa na
kusangalala.
21 Solomoni nakalongoza undewa weng'ha wa
kwaluchila lwanda lwa Eyufulate mbaka kuli isi
ya Wafilisti na kuli mbaka wa Misili. Wanhu wa isi
zeng'ha nawamkolela mijito na kulavya kodi kwa
heye kuli mhela weng'ha wa kikala kwa heye.

22 Chilyo choyatumiye Solomoni kuli zuwa
limwe nachali utimbo unojile lita elufu sita na
miya sita na utimbo wunji wa hihi hela lita elufu
kumi na zidatu na miya mbili
23 na misenga jinyatile kumi na misenga jilin-
gulya kisolo makumi meli na ming'holo miya
imwe, hamwe na ibala na chifuno na kulungu na
ng'huku zinojile lukami.
24 Kwa vila Solomoni nakalongoza undewa
weng'ha wa kolizinjilaga isanya mwa lwanda lwa
Eyufulate, kwaluchila Tifusa mbaka Gasa, ahyo
nayali na kikala goya kuli banzi zeng'ha.
25 Mazuwa geng'ha ga ulongozi wa heye
Solomoni kwa wanhu wa Yuda na wa Isilaeli,
kulawa Dani mbaka Beeli-sheba, nawekala kwa
kikala goya chila munhu hali migodi ja heye ja
mizabibu na mitini.
26 Solomoni nayali na vibumuli elufu makumi
gane (40,000) kwa chiwalo cha falasi na mituka
ja heye ja kubulunwa na wamizi wakwina falasi
elufu kumi na weli (12,000).

27 Wala vilongozi kumi na weli, chila yumwe
kuli mwezi woyalonjelwe, nawegala chilyo cha
kuhega kwa chiwalo cha mndewa Solomoni na

wanhu weng'ha walingulya hali chisaga cha mn-
dewa. Nawali wokweneza chila chinhu chilingu-
ganigwa.
28 Nawali wochigala kahi honhu ha vinhu vilin-
guganigwa vya shayili na misolo kwa chiwalo cha
falasi na kwa falasi wanji walingubilima lukami.

## *Luhala lwa mndewa Solomoni*

29 Nguluwi nakamha Solomoni luhala na ny-
hala ng'hatu na kuvizela lukami kuwele hakulin-
guweza kupimigwa kota sangalaza za mhwani.
30 Luhala lwa Solomoni nalwali lukulu kusinda
luhala lwa wanhu weng'ha wa kolilawila isanya
na kusinda luhala lwa wanhu wa Misili.
31 Nayali na luhala kusinda Etani, Mwesila na
kusinda Hemani na Kalikoli na Dalida, wana wa
Maholi. Lutogo lwa heye nalwenela kwa wanhu
wa isi zeng'ha za habehi.
32 Nakandika nhelo elufu zidatu (3,000) na nz-
imbo elufu imwe na zihano (1,005).
33 Nakalonga mbuli zilinguwala migodi,
kwaluchila mwelezi uwele Lebanoni na isopolo,
mizuchila jilingota kuli lukanzi. Nakalonga kahi
kuwala migongolo na videje na vilumbigwe
vilingutambala viwele na danda izizime
jilingulagaza mafinga, kota somba.
34 Wanhu wa isi zeng'ha nawoya kuhulichiza
luhala lwa Solomoni, wawele nawalajizwa
na wandewa weng'ha wa kuli isi zeng'ha
wawele nawahulika kuwala luhala lwa mndewa
Solomoni.

# 5

### *Solomoni kangiwika goya kuzenga ng'handa ya Nguluwi*

1 Mndewa Hilamu wa Tilo, loyahuliche kota
Solomoni nakabakalizwa mafuta leka yawe mn-
dewa honhu ha mhaza wa heye Daudi, nakalajiza
wasenga kwa Solomoni, kwa vila heye Hilamu
nayali goloko wa Daudi.
2 Solomoni nakahilika usenga kwa Hilamu yo-
longa,
3 "Kwanguvizela kota mhaza wa heni Daudi
nakalemwela kuzenga ng'handa ya kumfugamila
Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa heye, kwa chiwalo
cha kitowa ngondo na wang'honyo wa isi za
habehi mbaka hala Mkulu Nguluwi loyampele
kusumya.
4 Ila lelo, Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa heni,
nakamha heni kikala goya kuli banzi zeng'ha.
Haduhu mng'honyo ne magazo.
5 Lelo, nanhuwila kuzenga ng'handa kwa chi-
walo cha Mkulu Nguluwi, Nguluwi wa heni, kota
Mkulu Nguluwi vyoyamlonjele mhaza wa heni
Daudi, yolonga, 'Mwanago yondimuwika kuli
chigoda cha undewa honhu ha hegwe, ayo ndo
kozenga ng'handa kwa chiwalo cha itagwa lya
heni.'
6 Lelo, uwalajize wanhu wa hegwe wateme
mielezi ja Lebanoni kwa chiwalo cha heni.
Wanhu wa heni wokola mijito hamwe na wanhu
wa hegwe, nani ndowalipa vitumagwa wa
hegwe kota vyoulonga. Kwanguvizela kota

haduhu wanhu walingudaha kutema migodi
kota Wasidoni."
7 Hilamu loyahuliche usenga awo kulawa kwa
Solomoni, nakasangalala lukami na kulonga,
"Mkulu Nguluwi yatogoligwe lehano, kwa
vila nakamha Daudi mwana yawele na luhala
yawalongoze wanhu wa isi ayi ng'hulu."
8 Hamba, Hilamu nakalajiza usenga kwa
Solomoni, yolonga, "Nambochela usenga wa
hegwe wouulajize kwa heni, ndodita geng'ha
goulingugana leka ndikupe mizinga ja migodi ja
mielezi na mibeloshi.
9 Wanhu wa heni wojilavya mizinga ajo kulawa
Lebanoni mbaka mbahali, nani ndojiwoha kuli
vilundo mbaka honhu houlajila jilute. Ako ndo-
jidohola, nagwe kojibochela. Kokweneza kugana
kwa heni kwa kumha heni chilyo kwa chiwalo cha
wanhu wa kaye kwa heni."
10 Kwa nzila ayi, Hilamu nakamha Solomoni
migodi jeng'ha ja mielezi na mibeloshi kota vyoy-
aganile,
11 naye Solomoni nakamha Hilamu lita lachi
zine na elufu makumi gahano na zine (454,000)
za ngano na lita lachi zine na elufu makumi
gahano na zine (454,000) za mafuta ganojile ga
mzeituni, kwa chiwalo cha wanhu wa kaye kwa
heye. Solomoni nakalutilila kumditila ayi Hilamu
chila mwaka.
12 Mkulu Nguluwi nakamha Solomoni luhala
kota vyoyamlahile. Nakwali na kikala goya hali
Solomoni na Hilamu, weng'ha weli nawadita
ilagano hali hewo.
13 Mndewa Solomoni nakawakungajiza wanhu

elufu makumi gadatu (30,000) kulawa chila
honhu kuli isi yeng'ha ya Isilaeli, leka wakole
mijito ja kukola lupichi.
14 Nakawahilika wanhu Lebanoni kwa
kuwabagula kuli vilundo, wanhu elufu kumi
kuli chila mwezi, ahyo nawekala Lebanoni kwa
mwezi umwe na myezi mili nawekala kaye.
Adonilamu ndo nayali chilongozi wa wanhu
walingukola mijito kwa lupichi.
15 Solomoni nayali na vitumagwa wa kupika
mhomolo elufu makumi saba (70,000) na wahon-
gola maganga kuli vidunda elufu makumi nane
(80,000),
16 hamwe na vilongozi elufu zidatu na miya
zidatu wawele nawalongoza mijito ajo na
kuwalolela wakola mijito weng'ha.
17 Kwa mzilo wa mndewa, nawabawa maganga
makulu ga sendi nyinji, leka gahongoligwe na
kuzenjela msisi wa ng'handa ya Nguluwi.
18 Ahyo ndo walinguzenga wa Solomoni na wa
Hilamu na wanhu wa muji wa Gebali vyowa-
hongole maganga na kuwika goya mbawo kwa
chiwalo cha kuzenjela ng'handa ya Nguluwi.

# 6

### *Solomoni kanguzenga ng'handa ya Nguluwi*
### *(2 Mihela 3)*

1 Kuli mwaka wa miya zine na makumi nane
kulawa Waisilaeli lowalawile kuli isi ya Misili,
kuli mwaka wa kane wa ulongozi wa mndewa
Solomoni kuli Isilaeli, kuli mwezi wa Sifu, uwele
ndo mwezi wa keli, Solomoni nakaluka kuzenga
ng'handa ya Mkulu Nguluwi.

2 Ng'handa ayo iwele mndewa Solomoni
nakazenga kwa chiwalo cha Mkulu Nguluwi,
nayali na ulefu wa mita makumi meli na saba
na ugazi wa mita tisa na wimo wa mita kumi na
zidatu na nusu kuluta kuchanya.
3 Chituka cha kumwando nachali na ulefu wa
mita tisa, kwa kiwhana na ugazi wa ng'handa
ya Nguluwi na honhu halawilile kumwando kwa
ng'handa ayo nahali na ulefu wa mita zine na
nusu.
4 Nakaiwichila mitubuli migazi kwa mgati na
mizisili kwa kunze.
5 Nakagongomanya vihengo vya hafungo
kuizunguluta ng'handa ya Nguluwi yeng'ha
kwa wimo wa milingo jidatu kuluta kuchanya,
vihengo avyo navibatililwa na ng'hanzi za
ng'handa na za honhu helile.
6 Ilingo lya hasi nalyali na ugazi wa mita mbili
na lobo na ilingo liyage nalyali na ugazi wa
mita mbili na lobo zidatu na ilingo lya mchanya
ng'hatu nalyali na ugazi wa mita zidatu. Milingo
ajo najali jilivinji kwa ugazi, kwa vila Solomoni
nayali yapunguze lukanzi lwa kunze kuzunguluta
ng'handa, leka boliti za kwegamila ng'handa vi-
batane na lukanzi.
7 Mhela wa kuzenga ng'handa ya Nguluwi, ma-
ganga gahongoligwe hela ndo nagakola mijito
ajo, hakuwele na nyundo ne liwago ama chinhu
choneche cha chuma chiwele nachihulikwa kuli
honhu aho ha kuzenga ng'handa ya Nguluwi.
8 Lwizi lwa kwinjilila kuli ilingo lya hasi nal-
wali ubanzi wa kusini mwa ng'handa ya Nguluwi,
chikwinilo nachiluta kuli ilingo lya hagati na ku-
lawa aho nachiluta mbaka kuli ilingo lya kadatu.

9 Ahyo, Solomoni nakazenga ng'handa, naimala. Chinduwiko cha ng'handa nachali chigongomanyigwe kwa boliti na mbawo za mielezi.
10 Mndewa Solomoni nakazenga vihengo kuizunguluta ng'handa ya Nguluwi yeng'ha. Wimo wa chila chihengo nawali mita mbili na lobo na navyali vilumbile na ng'handa kwa boliti za mielezi.
11 Mhela awo, ulonzi wa Mkulu Nguluwi naumuyila Solomoni,
12 "Kuwala ng'handa ayi youlinguzenga, wone kowinza mzilo wa heni na kibatilila malajizo ga heni na malanguso ga heni, kwa kukolela hegwe ndokweneza kulagana kwa heni kondilagane na mhaza wa hegwe, Daudi.
13 Ndochikala hali Isilaeli na siwaleka wanhu wa heni, Isilaeli."
14 Ahyo, Solomoni nakazenga ng'handa ya Nguluwi na kusinda.

### *Vinoligo vya ng'handa ya Nguluwi*

15 Nakazigubika ng'hanzi zake za mgati kwa mbawo za mielezi, nakaziwika kuli ng'hanzi kulawa hasi ha ng'handa mbaka kuli chinduwiko na kuhagubika hasi ha ng'handa ya Nguluwi kwa mbawo za mibeloshi.
16 Chihengo cha mgati chilinguchemigwa honhu helile, nachizenjigwa kuli honhu ha kumbele ha ng'handa. Nachali chizenjigwe kwa mbawo za mielezi kulawa hasi mbaka kuli chinduwiko na ulefu wake nawali mita tisa.
17 Chihengo chikulu chiwele kumwando kwa honhu helile, nachali na ulefu wa mita kumi na nane.

18 Ng'handa ya Nguluwi kwa mgati nayali inoligwe kwa kiwhana na mayungu na uluwa ubawule. Chila chinhu nachali cha mielezi, hakuwele na iganga liwele nalyoneka.

19 Mgati mwa ng'handa ya Nguluwi nakagongomanya honhu helile ha mgati, kwa chiwalo cha kuliwika isanduku lya Ilagano lya Mkulu Nguluwi.
20 Honhu helile ha mgati nahali na ugazi wa mita tisa na ulefu wa mita tisa na wimo wa mita tisa. Honhu aho nahali hagubikwe kwa zahabu inojile na nakagongomanya honhu ha kulavila nhambiko kwa mbawo za migodi ja mielezi na kuhagubika kahi kwa zahabu inojile.
21 Solomoni nakahagubika honhu ha mgati ha ng'handa ya Nguluwi kwa zahabu inojile na nakawika migasi ja zahabu kulawa ubanzi umwe mbaka uyage uwele kumwando mwa honhu helile, hawele nahagubikwa kwa zahabu.
22 Ng'handa yeng'ha nakaigubika kwa zahabu inojile na honhu ha kulavila nhambiko kuli honhu helile kahi nakahagubika kwa zahabu inojile.

23 Hali honhu helile nakavigongomanya vilumbigwe vili viwele na mabawa kwa mbawo za mizeituni, chila chilumbigwe nachali na wimo wa mita zine na nusu.
24 Kuli chila ibawa lya chilumbigwe chiwele na mabawa, nalyali na ulefu wa mita mbili na lobo, lelo ulefu kulawa kuli kuduma kwa ibawa limwe mbaka kuduma kwa ibawa liyage nawali mita zine na nusu.
25 Chilumbigwe chiyage chiwele na mabawa

nachali na ulefu wa mita zine na nusu, vilumbigwe vyeng'ha vili navyali na vipimilo vivila na ukulu wuwula.
26 Wimo wa chila chilumbigwe chiwele na mabawa nawali mita zine na nusu.
27 Nakaviwika vilumbigwe avyo viwele na mabawa mgati mwa honhu helile ha ng'handa ya Nguluwi, mabawa ga vilumbigwe avyo nagali gagonzoligwe. Ibawa lya chilumbigwe chimwe nalyali lidoliza lukanzi lumwe, kuno ibawa lya chilumbigwe chiyage nalidoliza lukanzi luyage na mabawa ganji ga vilumbigwe avyo nagating'hana na kidoliza hagati ha chihengo.
28 Nakavigubika kwa zahabu vila vilumbigwe viwele na mabawa.
29 Mchanya mwa chila lukanzi lwa ng'handa ya Nguluwi nakunoligwa kwa kuhongoligwa vilumbigwe viwele na mabawa na migodi ja michikichi na uluwa ulingubawula.
30 Hanyi ha vihengo vyeng'ha vya mgati na vya kunze mwa ng'handa ya Nguluwi, nakahagubika kwa zahabu.
31 Hali honhu ha kwinjilila kuli chihengo cha mgati ng'hatu, nakagongomanya lwizi mili ja mbawo za mizeituni jiwele na wimo na fulemu zilingoneka ziwele na nzingo zihano.
32 Kuli lwizi ja mbawo za mizeituni nakanoliga kwa kuhongola vilumbigwe viwele na mabawa na migodi ja michikichi na uluwa ulingubawula, hamba nakagubika vinoligo avyo kwa zahabu.
33 Nakagongomanya kahi fulemu ziwele na nzingo zine kwa migodi ja mizeituni, kwa chiwalo cha lwizi mili ja chihengo chikulu.

34 Nakwali na lwizi jilinguweza kigonzola
jigongomanyigwe kwa mbawo za mibeloshi na
chila lwizi nalwali na bawaba zilinguweza kibina
kuli chila ubanzi mchanya mwa lwizi luyage.
35 Kuli lwizi ajo, nakahongola vilumbigwe vi-
wele na mabawa na migodi ja michikichi na
uluwa ubawule, nakajinoliga goya kwa zahabu.
36 Nakazenga lugagala lwa mgati, luwele
ng'hanzi zake nazali za misitali jidatu ja maganga
gahongoligwe na msitali umwe wa boliti za
mielezi.
37 Msisi wa ng'handa ya Mkulu Nguluwi nawali
uzenjigwe kuli mwaka wa kane na mwezi wa Sifu.
38 Kuli mwaka wa kumi na umwe, mwezi wa
Buli, uwele ndo mwezi wa nane, ng'handa ya
Nguluwi nayali isindile kuzenjigwa. Nakaizenga
ng'handa ayo kwa miyaka saba.

# 7

### *Ng'handa ya chiundewa ya Solomoni*

1 Solomoni nakazenga ng'handa ya heye ya chi-
undewa kwa mhela wa miyaka kumi na jidatu.
2 Hamba, nakazenga chihengo mgati mwa
ng'handa ya mndewa, chilinguchemigwa Chihulo
cha Lebanoni. Nachali na ulefu wa mita makumi
gane na zine na nusu na ugazi wake mita makumi
meli na mbili na lobo na wimo wake nawali
mita kumi na zidatu na nusu. Chihengo acho
nachali chizenjigwe mchanya mwa misitali jine ja
mizengo ja mielezi, mizengo jiwele najali jibatilile
boliti za mielezi kwa ubanzi wa kuchanya.
3 Chila msitali nawali na mizengo kumi na
jihano, ahyo jeng'ha hamwe najali mizengo

makumi gane na jihano. Vihengo vizenjigwe mchanya mwa mizengo ajo, nakaviwichila vinduwiko vya mbawo za mielezi.

4 Nakwali na misitali jidatu ja mitubuli jilingilola.

5 Lwizi jeng'ha najali ja nzingo zine, najali ubanzi wa kumwando kuli misitali jidatu, jichilola.

6 Nakazenga lugagala lwa mizengo, ulefu wake nawali mita makumi meli na lobo na ugazi wake nawali mita kumi na zidatu na nusu. Hali honhu ha kumwando ha lugagala alo nakwali na chituka na kumwando mwa chituka acho nakwali na mizengo na chinduwiko chidodo.

7 Solomoni nakazenga chitala cha chigoda cha undewa, hawele amo nayali yotagusa wanhu. Chitala acho nachichemigwa Chitala cha Utaguso. Nachali chinoligwe kwa mbawo za mielezi kulawa hanyi mbaka kuli chinduwiko.

8 Ng'handa ya kikala heye, iwele nayali kumbele kwa Chitala cha Utaguso nayali izenjigwe kota ziyage. Solomoni kahi nakazenga ng'handa kota ayo kwa chiwalo cha mhinza wa Falao, yawele nayali yamhesile.

9 Ng'handa azo zeng'ha nazizenjigwa kwa maganga ga sendi nyinji kulawa kuli msisi mbaka kuchanya, maganga gahongoligwe kwa vipimilo vyowaganile na kudumuligwa kwa msumeno banzi zeng'ha.

10 Msisi nawali wa maganga ga sendi nyinji na makulu gawele na ulefu wa mita zidatu na nusu na ugazi mita zine na nusu.

11 Honhu ha kuchanya nahazenjigwa kwa mag-
anga ganji gahongoligwe kwa vipimilo vivila vy-
owaganile na kwa mbawo za mielezi.
12 Lugagala lwa ng'handa ya mndewa nalwali
na lukanzi luwele na msitali umwe wa mbawo za
mielezi jipanjigwe mchanya mwa misitali jidatu
ja maganga ga kuhongola, kota vyoluwele luga-
gala lwa mgati mwa ng'handa ya Mkulu Nguluwi
na chituka chake.

### *Mijito ja Hilamu*

13 Mndewa Solomoni nakawalajiza wanhu ku-
migala Hilamu kulawa Tilo.
14 Hilamu, nayali mwana wa mdala yafililwe na
mlume wa heye, kulawa nhanzi ya Nafutali na
mhaza wa heye nayali mwenyeng'haye wa Tilo,
mponda shaba. Hilamu nayali na kuvizela na
muwanzi ng'hatu wa mijito joneche ja shaba, lelo
nakaluta kwa mndewa Solomoni, nakamkolela
mijito ja heye jeng'ha.

### *Mizengo mili ja shaba ya ng'handa ya Nguluwi (2 Mihela 3:15-17)*

15 Hilamu nakagongomanya mizengo mili ja
shaba, chila limwe nalyali na ulefu wa mita nane
na mzunguluto wake mita zihano na nusu.
16 Nakagongomanya mitaji mili ja shaba, chila
limwe nalyali na ulefu wa mita mbili na nusu
kuluta kuchanya, nakajiwika mchanya mwa
mizengo ajo.
17 Hamba, nakagongomanya migasi jibotigwe
kuli jila mitaji mchanya mwa jila mizengo.
Nakwali na migasi saba kuli chila itaji.

18 Nakagongomanya mafuza ga mako-
mamanga, nakagawika kuli misitali mili
kujizunguluta jila mitaji mchanya mwa chila
izengo.
19 Mitaji jiwele mchanya mwa mizengo ja chi-
tuka, najali jikoneka kota uluwa wa yunjiyunji na
wimo wake nawali mita imwe na lobo zidatu.
20 Mitaji ajo najali mchanya mwa ajo mizengo
mili na najali kahi mchanya mwa honhu halingi-
whana na chisaye. Habehi na wula utandawala
nakwali na gala makomamanga miya mbili kuli
misitali kuzunguluta chila itaji.
21 Hilamu nakajiwika mizengo ajo kuli chituka
cha ng'handa ya Nguluwi, izengo lyoyalimize
ubanzi wa kusini nalichemigwa Yakini* na lila
lyoyalimize ubanzi wa kasikazini nalichemigwa
Boasi†.
22 Mitaji jiwele kuchanya najali jikoneka kota
uluwa wa yunjiyunji. Ahyo mijito ja mizengo ajo
najali jisindile.

### *Ibiga lya shaba*
### *(2 Mihela 4:2-5)*

23 Hamba Hilamu nakagongomanya ibiga
lya shaba lilinguchemigwa Bahali. Nalyali lya uvilingo liwele na ugazi wa mita zine na nusu kulawa nzingo imwe mbaka nzingo iyage na wimo wa mita mbili na lobo na mzunguluto wa mita kumi na zidatu na nusu.

* **7:21 7:21** *Yakini* Ulonzi awu kwa Chiebulaniya una mana Nguluwi kodita nzinzili. † **7:21 7:21** *Boasi* Ulonzi awu kwa Chiebulaniya una mana kwa mong'ho wa Nguluwi.

24 Hasi ha nzingo yake nakuzungulutwa
na misitali mili ja mayungu, mayungu kumi
kuli chila sentimita makumi gane na zihano.
Mayungu ago nagagongomanyigwa mhela
wuwula wa kuligongomanya ibiga.
25 Ibiga alyo nalyali liwichigwe mchanya mwa
jimalukolo ja mibuguma kumi na mili, jidatu na-
jilola kasikazini na jidatu jinji najilola kolizinji-
laga isanya na jidatu kahi najilola kusini na jidatu
jiyage najilola kolilawilaga isanya. Ibiga alyo nali-
wichigwa mchanya mwa mibuguma ajo honhu
hawo ha kumbele.
26 Nzingo zake nazali na ugazi wa sentimita
saba na nusu na nazali ziwhana na nzingo za
chizombe na kota wula uluwa wa yunjiyunji.
Ibiga alyo nalyali liweza kuwichigwa mazi lita
elufu makumi gane (40,000).

### *Mituka ja shaba*

27 Hilamu kahi nakagongomanya mituka kumi
ja shaba, chila mutuka nawali na ulefu wa mita
imwe na lobo zidatu na ugazi wa mita imwe na
lobo zidatu na wimo wa mita imwe na lobo.
28 Mituka ajo najigongomanyigwa hino.
Nakwali na mabamba ga hafungo gawele nagali
gabatililwe na fulemu.
29 Mchanya mwa mabamba na hagati ha azo
fulemu, nakwali na jimalukolo ja misimba na
mibuguma na vilumbigwe viwele na mabawa.
Mchanya na hasi ha misimba na mibuguma
nakwali kuwichigwe vinoligo vya kupondigwa.
30 Chila mutuka nawali na magulududumu gane
ga shaba na vinhu vya hagati vya kugazungulusila

maguludumu ago navyali vya shaba. Kuli nzingo
zine za mutuka nakwali na vibatililo vya shaba
kwa chiwalo cha ibiga. Habehi na chila chibatililo
nakwali na vinoligo vya kupondigwa.
31 Honhu ha kuchanya ha mutuka nahali
mwanzi na ha mvilingo, nahaluta kuchanya
kwa nusu mita na sentimita kumi na nane mgati
mwake. Kwa kunze, honhu hala nahanoligwa,
mabamba gake nagali ga mlaba hagawele ga
mvilingo.
32 Maguludumu ago gane nagali hasi ha
mabamba na vinhu vya hagati vya kuzungulusila
maguludumu, navyali vilumbile na fulemu na
wimo wa maguludumu ago nawali sentimita
makumi sita na sita.
33 Maguludumu ago nagagongomanyigwa kota
maguludumu ga mituka ja ngondo ja kukwejigwa,
mvilingo wake na chila chinhu cha maguludumu
ago nachali cha kupondigwa.
34 Chila fulemu nayali na moko gane. Moko
umwe kuli chila nzingo.
35 Mchanya mwa chila mutuka nakwali na
fito ilingudita uvilingo wa wimo wa sentimita
makumi meli na mbili. Vibatililo vyake na
mabamba gake gawele ubanzi wa kuchanya, nav-
ilumba na mutuka.
36 Moko na mabamba navinoligwa kwa ji-
malukolo ja vilumbigwe viwele na mabawa na
misimba na migodi ja michikichi mchanya mwa
fito, hamwe na mitaji jibotigwe kuzunguluta
honhu heng'ha.
37 Ahi ndo Hilamu vyoyagongomanye jila mi-
tuka kumi. Jeng'ha najali ja kugongomanyigwa

kwa kupondigwa, jiwele na vipimilo na ukulu vilingiwhana.

38 Hamba nakagongomanya mibiga jinji kumi ja
shaba, ibiga limwe kuli chila mutuka. Chila ibiga nalyali na ugazi wa mita imwe na lobo zidatu na naliweza kuwika mazi lita miya nane.
39 Nakawika mituka jihano kuli ubanzi wa
kusini wa ng'handa na mituka jihano kuli ubanzi wa kasikazini na lila ibiga likulu nakaliwika kuli ubanzi wa kusini kolilawilaga isanya mwa yila ng'handa.

## *Vinhu vya ng'handa ya Nguluwi (2 Mihela 4:11-5:1)*

40 Hilamu nakagongomanya kahi mibiga na
makoleo na visaye vya kumizila. Lelo, Hilamu nakasinda mijito jeng'ha joyawele yomkolela mndewa Solomoni kuli ng'handa ya Mkulu Nguluwi,
41 mizengo mili na mitaji mili jilingiwhana na
visaye navyali mchanya mwa mizengo na utandawala wili kwa chiwalo cha kunoliga ajo mitaji mili jilingiwhana na visaye, jiwele mchanya mwa mizengo
42 na makomamanga miya zine kwa chiwalo
cha utandawala awo wili na misitali mili ja makomamanga kwa chila utandawala leka kunoliga jila mitaji mili jilingiwhana na visaye, jiwele mchanya mwa mizengo.
43 Nakagongomanya kahi vikalilo kumi hamwe
na nyhelo kumi kuli mituka ajo
44 na lila ibiga likulu na jila mibuguma kumi na
mili hasi ha ibiga

45 na mibiga na makoleo na visaye vya ku-
mizila. Vinhu avi vyeng'ha viwele Hilamu nakam-
gongomanyila mndewa Solomoni kwa chiwalo
cha ng'handa ya Mkulu Nguluwi, navyali vya
shaba ilingupulika.
46 Vinhu avyo vyeng'ha mndewa nakavigongo-
manya kuli ibindi lya Yolodani, honhu hawele na
misanga ja ilongo lya kulumbila vinhu, hawele
hagati ha Sukoti na Saletani.
47 Solomoni nakavileka vinhu avyo ne kuvip-
ima kwa vila navyali vinji lukami, itunyo lya
shaba haliwezile kuzeleka.
48 Solomoni nakagongomanya kahi vinhu
vyeng'ha viwele kuli ng'handa ya Mkulu Nguluwi,
viwele ndo honhu ha kulavila nhambiko ha
zahabu na chisaga cha zahabu kwa chiwalo cha
mibumunda ja kuwika hali Nguluwi
49 na vinhu vya kuwichila chenje vya zahabu
inojile viwichigwe kumwando ha honhu helile
ng'hatu, vihano kuli ubanzi wa kusini na vihano
kuli ubanzi wa kasikazini, kumwando ha honhu
helile ng'hatu. Nakagongomanya kahi uluwa na
vyenje na makoleo
50 na vizombe na mikasi ja kudumulila tambi
za mishumaa na visaye vya kumizila na vifunyizi
vya ubani na bawaba kwa chiwalo cha lwizi lwa
honhu helile ng'hatu na kwa chiwalo cha lwizi
lwa chituka chikulu cha ng'handa ya Nguluwi.

51 Lelo mndewa Solomoni loyasindile mijito
jeng'ha kuli ng'handa ya Mkulu Nguluwi, nakavi-
wika mng'handa vila vinhu viwele Daudi, mhaza
wa heye nayali yaviditile viwe vya chiuyeng'ha,
viwele ndo sendi na zahabu na vinhu viyage,

hamba nakaviwika vinhu avyo kuli ng'hano za ng'handa ya Mkulu Nguluwi.

# 8

*Isanduku lya ilagano lyangugaligwa kuli ng'handa ya Nguluwi*
*(2 Mihela 5:2-6:2)*

1 Lelo, mndewa Solomoni, nakawachema
wasekulu na vilongozi weng'ha wa nhanzi na wa ivyazi lya Isilaeli ako Yelusalemu, leka waligale isanduku lya ilagano lya Mkulu Nguluwi kulawa honhu hamwenga ha muji wa Daudi, hawele ndo chidunda cha Siyoni mbaka kuli ng'handa ya Nguluwi.
2 Walume weng'ha wa Isilaeli nawekungajiza
kwa mndewa Solomoni mhela wa mnvina ya vibumuli, kuli mwezi wa Etanimu, uwele ndo mwezi wa saba.
3 Wasekulu weng'ha wa Isilaeli lowafichile,
watambika nawalipika isanduku lya ilagano lya Mkulu Nguluwi.
4 Walawi na watambika nawalihola isanduku
lya ilagano lya Mkulu Nguluwi na ihema lya Nguluwi na vinhu vyelile vyeng'ha viwele amo mihema, watambika na Walawi nawavipika.
5 Mndewa Solomoni na nhing'hano yeng'ha
ya Waisilaeli wawele nawekungajiza hali heye, wawele nawali hali alyo isanduku lya ilagano, nawalavya nhambiko nyinji za ming'holo na misenga jiwele hisabu yake hailinguweza kwandichigwa ne kuwazigwa.
6 Hamba watambika nawalihilika isanduku lya
ilagano lya Mkulu Nguluwi mbaka hali honhu

hake, mgati mwa honhu helile ha ng'handa ya Nguluwi, hawele ndo honhu helile ng'hatu, nawaliwika hasi ha mabawa ga vilumbigwe viwele na mabawa.
7 Avyo vilumbigwe viwele na mabawa navigonzola mabawa gawo mchanya mwa honhu hawichigwe isanduku lya ilagano, ahyo isanduku alyo na mipichilo jake navyali hasi ha mabawa.
8 Mipichilo jake najali ng'wemang'wema lukami mbaka najoneka kulawa honhu helile hali honhu helile ng'hatu, ila hajilingoneka hanze ha honhu helile. Mipichilo ajo jing'hali kuko.
